SIKU YA KIMATAIFA YA MAOMBI KWA WAATHIRIKA
WA USAFIRISHAJI HARAMU WA BINADAMU 2023

TUME YA KIMATAIFA YA HAKI ZA BINADAMU

JESHI LA WOKOVU

# NIMESIKIA VILIO VYAO



## MSAADA WA KUJIFUNZA BIBLIA

Umeandikwa na **Kamishena Prema Wilfred (R)**
*Teritori ya India Kusini Magharibi*

**‘Wana wa Israeli wakaugua kwa sababu ya ule utumwa, wakalia, kilio chao kikafika juu kwa Mungu kwa sababu ya ule utumwa. Mungu akasikia kuugua kwao, Mungu akakumbuka agano lake alilolifanya na Ibrahimu na Isaka na Yakobo.’ (Kutoka 2:23-25).**

### UTANGULIZI

Haijalishi ni wapi tunaishi duniani, utumwa wa kileo na usafirishaji haramu wa binadamu unatendeka kutuzunguka. Unatendeka majumbani, katika majirani, vijijini na katika miji kote katika nchi zetu.

**SHUGHULI YA KIKUNDI** *Dakika 15*

Unafahamu nini kuhusu utumwa wa kileo na usafirishaji haramu wa binadamu? Katika vikundi vidogo, andika chini na jadili yote uyajuayo kuhusiana na haya. Chukua muda kushirikishana katika kundi kubwa yale yaliyojadiliwa katika kila kikundi kidogo.

### UTUMWA NI NINI?

Utumwa ni pale ambapo mtu humtawala mtu mwingine kama yule mtu ni kitu au ni mali yake. Utawala huo hutegemea tishio au matumizi ya ukatili iwe ni kimwili, kihisia, kisaikolojia, kiroho au kifedha. Wakati watu wanapitia utumwa, wananyanyaswa. Hii maana yake ni kwamba wanatendewa isivyo haki kwa manufaa ya kibinafsi ya mtu mwingine.

Watu walio katika utumwa wanadhalilishwa na kutendewa kama wao ni vitu. Utu wao na uwezo wa kufanya maamuzi wananyang’anywa. Vikwazo vinawekwa kila sehemu ya maisha yao. Wanalazimishwa kutoa sadaka tumaini lao, ndoto zao, wapendwa wao, mambo yao ya nyuma na ya mbeleni. Kama wanalipwa kwa kazi zao, huwa sio kiwango cha kutosheleza kuishi. Huwanyang’anya uhuru wao na ni ukiukaji wa haki zao za ubinadamu.

Makisio ya dunia ya mwaka 2022 yanaonyesha kwamba idadi kubwa ya watu wanaopitia utumwa wa kileo na usafirishaji haramu wa binadamu imeongezeka kwa makisio ya watu milioni 49.6 kwa siku yoyote.

Hii maana yake wastani duniani:

- Watu milioni 27.6 wanapitia kazi za kulazimishwa na unyanyasaji wa kingono.
- Watu milioni 22 wanapitia ndoa za kulazimishwa.

## UTUMWA UNAFANANAJE KOTE DUNIANI ?

Utumwa unaweza kuwa na sura nyingi mbalimbali kote duniani. Hapa kuna mifano kadhaa:

Baba yake na Klenam* alipoteza kazi kijijini kwao. Familia ilikuwa kubwa yenye watoto wengi wa kulisha. Wakati jirani alipomtambulisha Klenam kwa mtu aliyemwahidi kazi ya mshahara mzuri na nafasi ya kumaliza shule, alifikiria nafasi hii itasaidia familia yake. Alipofika huko tu, hakwenda shule. Badala yake, alifanya kazi kwa masaa 12-14 kila siku kwenye boti ya uvuvi wa uduvi, wakizamia chini ya maji kuzikwamua nyavu huku hapati malipo na kupewa chakula kidogo kwa kazi yake ya hatari.

Familia ya Fatemeh* ilikimbia jiji lao wakati wanamgambo walipovamia jiji lao wakaanza kuwashambulia wanaoishi humo. Wakiwa wamehamishwa na wanaishi katika kambi ya wakimbizi, baba yake na Fatemeh alimwoza licha ya Fatemeh kuiambia familia yake kwamba hakutaka kufanya hivyo. Sasa, mume wake ambaye ana umri mkubwa zaidi na mama mkwe wake wanatawala sehemu zote za maisha yake na wanafaidika na kazi anazozifanya hapo nyumbani.

Rafiki wa kiume wa Sally* ni mzuri na mchangamfu. Anampa zawadi mda wote. Anamfanya Sally ajisikie anapendwa na anakubalika. Sally amekuwa siku zote akitafuta mahali atakapopaita nyumbani na mtu ambaye atamtunza. Baada ya majuma kadhaa ya haya kufanyika, rafiki yake wa kiume akamwambia anatakiwa amlipe na amsaidie kwa kufanya tendo la ndoa na marafiki zake. Alipojaribu kukataa na kuondoka, rafiki yake huyo alikuwa katili kwake na akatishia ataiumiza familia yake Sally.

* Jina limebadilishwa ili kumlinda.

## BIBLIA INASEMA NINI?

Kutoka 2:23-25

**Utangulizi:**

Kitabu cha Kutoka kinasisitiza kwamba Mungu hasimami pembeni mwa historia lakini yupo kazini akijishughulisha na kuwahukumu wakandamizaji na kuwakomboa wanaokandamizwa. Kinasisitiza kwamba yeye ni mwenye nguvu zaidi kuliko watawala wa hapa duniani. Kutoka inadhihirisha wazi kwamba yeye ndiye Mungu anayewakomboa watu kutoka kwenye utumwa wa aina zote na huwaletea wokovu, tumaini, uponyaji, furaha na ukombozi.

## MASWALI YA KUJADILIANA

- Wayahudi walikuwaje watumwa Misri?
- Unafahamu nini kuhusu hadithi ya Yusufu katika Mwanzo?

Mwanzo wa Kutoka unatusaidia kuelewa hali iliyowakabili wana wa Israeli ilivyokuwa – mapambano yao, ukandamizaji wao na utumwa wao Misri. Tunapotizama nyuma katika historia ya Israeli katika nchi hii ya kigeni, ilikuwa ni kwa sababu ya usafirishaji haramu wa binadamu wa Yusufu, aliyeuzwa utumwani na kaka zake. Alipokuwa mtumwa wa Farao, Yusufu alipitia magumu mengi, uchungu na ukandamizaji. Hata hivyo Mungu alikuwa na kusudi na maisha ya Yusufu. Mungu alimkomboa Yusufu kutoka kwa mapambano yake akamwinua kufikia ngazi ya juu ya uongozi Misri. Yusufu aliwasamehe kaka zake wakati wa njaa na akawasaidia kuhamia Misri.

Baada ya Yusufu kufariki na Farao mpya akaingia madarakani, Wamisri waliwaogopa Waebrania waliokuwa wanaongezeka kwa kasi ndani ya nchi yao na kwa makusudi wakatafuta kuwaua watoto wa kiume wa Waebrania wanaozaliwa. Lakini Mungu aliingilia kati akamwokoa Musa kwa ajili ya kusudi lake. Kuona kwamba bado Waisraeli walikuwa wanaongezeka kwa kasi kiidadi, Wamisri waliwalazimisha kufanya kazi – utumwa. Hata kama Waisraeli walikuwa sasa

raia wa Misri na walikuwa wanafanya kazi ya kujenga na kuiboresha nchi, lakini bado walikuwa hawahesabiwi kuwa binadamu na haki zao walinyang'anywa. Walikandamizwa – maisha yao yalijaa ugumu usio na haki, walikosa usawa, maumivu na uchungu. Hakuwepo mwenye uwezo wa kuzikabili nguvu za Farao au kupambana kupata haki. Kutokana na uchungu na maumivu yao, 'waliugua katika utumwa, wakamlilia Mungu' (Kutoka 2:23).

## MASWALI YA KUJADILIANA

**Mungu alijibu namna gani kilio cha Waisraeli?**

Sura ya 2:24-25 inaelezea majibu ya Mungu kwa kilio cha watu wake.

- Alisikia kuugua na kulia kwao – katika tafsiri ya (New International Version), neno 'kuugua' linaunganisha kwa karibu na wazo la 'kulia kwa sauti'. Waebrania wakati huo hawakuwa na kiongozi – hawakuwa na wa kumgeukia. Kabisa walikuwa hawana uwezo na walikuwa hawana matumaini. Kile walichoweza kufanya kilikuwa ni kulia kwa Mungu tu. Vilio vyao havikuenda kwa miungu ya wapagani bali kwa muumba wa dunia hii na wanadamu wote. Vilio vyao vilipaa kwake Mungu wa baba zao. Zaburi 50:15 inasema, 'ukaniite siku ya mateso, nitakuokoa, na wewe utanitukuza.' Mungu husikia kilio cha watu wote.
- Alikumbuka agano lake - Neno 'alikumbuka' Kiebrania ni 'Zakar' ambayo ni kiini muhimu cha kitheolojia katika kitabu cha Kutoka. Katika Kiebrania, kukumbuka sio tu ni zoezi la kiakili bali ni pamoja na kuchukua hatua kwa kumbukumbu hiyo. Mungu alikuwa amefanya ahadi zisizo na masharti kwa Ibrahimu na vizazi vyake. Tofauti na wanadamu, Mungu ni mwaminifu. Hasahau ahadi alizozitoa. Atazikamilisha hata kama kwetu inaonekana anachukua muda mrefu kuzitekeleza.
- Alihusika – Mungu sio tu alisikia na akakumbuka lakini vile vile alihusika. Mungu wa Israeli hakuwa hafahamu kuhusu hali mbaya ya watu wake au hakuwa tayari kuwaokoa kutoka kwenye ukandamizaji. Alikuwa anapanga kufanya jambo fulani ili kuwaokoa kutokana na utumwa waliokuwa wanakabiliana nao Misri. Vitendo hivi vya kusikia, kukumbuka na kuhusika vilikuwa ishara za uaminifu na huruma zake kwa uumbaji wake.

Vifungu hivi tunavyovisoma katika kitabu cha Kutoka vinatwambia kwamba watu duniani kote wanaopitia utumwa hawako peke yao. Mungu anasikia vilio vyao kutoka katika giza lao, anakumbuka naye anahusika anapofanya ili kuwaleta wote katika mwanga wake.

'Vilio vyao vya kutaka msaada havikuenda kwa miungu ya wapagani bali kwa **Muumba wa dunia** hii na wanadamu wote'.